


# MSUKUMO KUELEKEA USAWA:

## MATOKEO YA UTAFITI WA KIMATAIFA KUHUSU WANAUME NA USAWA WA KIJINSIA (IMAGES) - TANZANIA

**KUHUSU UTAFITI HUU**

Utafiti wa Kimataifa Kuhusu Wanaume na Usawa wa Kijinsia nchini Tanzania (The International Men and Gender Equality Survey - IMAGES) ulihusisha ukusanyaji wa taarifa za kitakwimu (*quantitative*) za watu wenye miaka 15 hadi 49, pamoja na utafiti uliolenga kupima ubora (*qualitative*) uliohusisha vijana wenye miaka 15-24. Promundo-US ilifanya utafiti huu kwa kushirikiana na Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania (UMATI) na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS). Washirika wa utafiti huu ni pamoja na Economic Development Initiatives (EDI) na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP).

**KUHUSU UTAFITI WA KIMATAIFA JUU YA WANAUME NA USAWA WA KIJINSIA (IMAGES)**

Utafiti wa Kimataifa Kuhusu Wanaume na Usawa wa Kijinsia (IMAGES) ni utafiti wa kina unaofanyika katika nchi kadhaa na kuangalia, pamoja na mambo mengine, hali halisi miongoni mwa wanaume na wanawake, mienendo na mitazamo kuhusu masuala ya kijinsia, sera zenye lengo la kuleta usawa wa kijinsia, mamlaka katika ngazi ya kaya, ushiriki wa akinababa katika matunzo na malezi ya watoto, ukatili wa majumbani, tofauti za kijinsia, afya, changamoto za kiuchumi na masuala mengine. Promundo na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Masuala ya Wanawake (International Center for Research on Women) walianzisha utafiti huu mwaka 2008. Hadi 2018, Utafiti wa IMAGES na tafiti nyingine zilizotokana na IMAGES zimefanyika katika nchi zaidi ya 40, na nyingine zaidi ziko mbioni kufanyika. IMAGES kwa kawaida hufanyika sambamba na kupima kiwango (*qualitative*) cha mfumodume, kupata matokeo yanayoendana na mazingira, na kutoa historia za kina za maisha ya watu ambazo zinasaidia kupata mwangaza/maelezo zaidi katika matokeo ya kitakwimu (*quantitative*). Dodoso linalotumika hurekebishwa ili liendane na mazingira ya nchi na eneo husika, ambapo takriban theluthi mbili ya maswali yanafanana kwa kila mahali. Kwa taarifa zaidi tazama: www.promundoglobal.org/images.

**WAANDISHI**

Ruti Levtov, *Mkurugenzi wa Tafiti, Tathmini na Mafunzo, Promundo-US*
Kristina Vlahovicova, *Afisa Tafiti, Promundo-US*
Gary Barker, *Rais na Afisa Mtendaji Mkuu, Promundo-US*
Ellen Stiefvater, *Mtaalam wa Utafiti, Promundo-US*
Lugano Daimon, *Mkurugenzi Mtendaji, UMATI*
Aroldia D. Mulokozi, *Afisa Tafiti, TACAIDS*

**UFADHILI**

Utafiti huu umefadhiliwa na - Bill & Melinda Gates Foundation. Matokeo na mahitimisho yaliyofikiwa katika utafiti huu ni ya waandishi na hayana uhusiano wa moja kwa moja na mitazamo au sera za Bill & Melinda Gates Foundation.

**KWA JILI YA KUNUKUU UTAFITI HUU:**

Levtov, R., Vlahovicova, K., Barker, G., Stiefvater, E., Lugano, D., na Mulokozi, A. D. (2018). *Msukumo Kuelekea Usawa: Matokeo ya Utafiti wa Kimataifa Kuhusu Wanaume na Usawa wa Kijinsia Tanzania (IMAGES): Muhtasari*. Washington, DC: Promundo-US, Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania, na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

© Promundo-US, 2018.

**DESIGN AND LAYOUT:** Blossom | blossoming.it

MUHTASARI

# MSUKUMO KUELEKEA USAWA:

## MATOKEO YA UTAFITI WA KIMATAIFA KUHUSU WANAUME NA USAWA WA KIJINSIA (IMAGES) - TANZANIA

2018

# MUHTASARI

**Licha ya juhudi kubwa zinazofanyika nchini Tanzania — kama ilivyo sehemu nyingi duniani — kumeendelea kuwepo na tatizo la ukosefu wa usawa wa kijinsia na athari zake**. Tanzania ni nchi ya 129 kati ya nchi 159 kwenye orodha ya Nchi Zisizokuwa na Usawa wa Kijinsia iliyotolewa na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa mwaka 2015 (United Nations Development Program's 2015 Gender Inequality Index). Viwango vya ukatili dhidi ya wanawake havijabadilika tangu 2010 hadi 2015 (ICF, 2015), na bado kuna tofauti kati ya wanawake na wanaume kwenye viwango vya uwezo wa kusoma na kuandika, uandikishwaji shuleni na ufaulu katika shule za sekondari na taasisi za elimu ya juu (UNICEF, 2011), kama ambavyo bado kuna kiwango kikubwa cha mahitaji ya huduma za uzazi wa mpango ambacho hakijatoshelezwa pamoja na tatizo la mimba za utotoni, ndoa katika umri mdogo na ukatili dhidi ya watoto (MoHCDGEC et al.., 2016; UNICEF, CDC&MUHAS, 2011).

**Chimbuko la matatizo haya ni matarajio ya kijinsia, desturi na tofauti za ki-mamlaka, mambo ambayo huchochea mitazamo, tabia na fursa**. Lengo la Utafiti wa Kimataifa Kuhusu Wanaume na Usawa wa Kijinsia Tanzania (IMAGES) ni kutoa takwimu na taarifa zitakazosaidia kufahamu namna jinsia na mfumo dume vinavyoathiri ustawi na maendeleo kwa kiasi kikubwa. IMAGES Tanzania inahusisha ukusanyaji wa taarifa za kitakwimu (*quantitative*) uliofanyika kwa wanawake na wanaume zaidi ya 2,000 wenye miaka 15 hadi 49 pamoja na utafiti unaolenga kupima ubora (*qualitative*) uliohusisha vijana wenye miaka 15-24. Utafiti huu ni wa kipekee katika namna kadhaa: Ni utafiti wa kwanza wa IMAGES duniani uliohusisha watu wenye umri chini ya miaka 18, uliokusanya taarifa za kiasi cha muda ambao watu wanatumia katika kufanya jambo fulani, na kujikita katika kupima mitazamo ya kijinsia kwenye jamii na pia kuangalia mitazamo binafsi.

## MATOKEO YA IMAGES TANZANIA

**Matokeo ya IMAGES Tanzania yanaonesha kwamba bado kuna kazi kubwa ya kupambana na kubadilisha mfumo dume na kupandisha hadhi na nafasi ya wanawake na wasichana katika jamii za Kitanzania**. Kama ilivyo katika matokeo ya tafiti za usawa wa kijinsia duniani kote, matokeo ya IMAGES Tanzania yanathibitisha kuwepo kwa uhusiano kati ya namna jamii inavyowachukulia na kuwathamini wanawake na wasichana na uwezo wao wa kuwa na mamlaka juu ya miili yao, kupata haki za kisheria, afya, uwezo wa kufanya maamuzi na maeneo mengine mengi. IMAGES Tanzania inaainisha namna wanaume na wavulana wanavyoathiriwa na ukosefu wa usawa wa kijinsia tangu utotoni hadi wanapokuwa watu wazima.

**Kwa mitazamo ya kijinsia, wanaume wengi na wanawake wengi zaidi kwa ujumla wanataka kuwepo kwa usawa wa kijinsia**. Asilimia 21 tu ya wanaume na asilimia 16 tu ya wanawake ndio wanaohisi

kwamba “wanawake wakipewa haki zaidi, wanaume wanashuka hadhi/daraja,” na chini ya asilimia 18 ya wanaume na asilimia 13 tu ya wanawake ndio wanaohisi kwamba wanawake wanapofanya kazi wanawanyang’anya wanaume fursa za kazi.

**Hata hivyo, wanaume na wanawake hawaungi mkono usawa linapokuja suala la mahusiano ya kawaida ya kila siku baina ya wanawake na wanaume** — kwa maana ya majukumu ya kijinsia katika kaya, mamlaka na uwezo wa kufanya maamuzi, ukatili dhidi ya wanawake, ujinsia na uzazi na mitazamo kuhusu jinsi na tofauti za kijinsia. Kwa mfano, asilimia 71 ya wanawake na 63 ya wanaume wanaamini kwamba jukumu muhimu zaidi la mwanamke ni kuangalia nyumba na kupikia familia; takriban asilimia 90 ya watu waliohojiwa walisema hawawezi kuwa na urafiki na mwanaume anayejihusisha na mapenzi ya jinsi moja na kwamba wangepata aibu endapo wangekuwa na mtoto wa kiume anayejihusisha na mapenzi ya jinsi moja.

**Mitazamo, matendo na hali za wanaume na wanawake, zinajengwa kwa kiasi fulani na mambo waliyoyapitia tangu utotoni, yawe mazuri au mabaya**. Katika utafiti wa IMAGES Tanzania, wanaume na wanawake wana kumbukumbu tofauti kuhusu mienendo ya uhusiano katika kaya walizokulia. Wanaume walikuwa na uwezekano mkubwa wa kuhusisha mamlaka ya kufanya uamuzi na baba zao (au wenzi wa mama zao) kuliko wanawake, kwa mfano, takriban theluthi mbili walisema mwanaume ndiye aliyekuwa mwenye uamuzi wa mwisho katika kufanya manunuzi ya vitu vikubwa kama pikipiki, ng’ombe au ardhi, ukilinganisha na takriban chini ya nusu ya wanawake walioripoti hivyo. Wakati huo huo, idadi kubwa ya wanaume kuliko wanawake waliripoti kwamba baba zao au wanaume wengine katika familia walizokulia waliwahi kushiriki katika kufanya kazi mbalimbali za nyumbani; asilimia 54 ya wanaume na 42 ya wanawake waliripoti kwamba baba zao waliwahi kushiriki katika angalau kazi moja kati ya nne za nyumbani zinazochukuliwa kwamba “ni za kike”.

**Wanaume na wanawake wana maoni yanayotofautiana sana juu ya baadhi ya masuala yanayohusu afya ya uzazi na ujinsia**. Namna watu walivyoelezea historia zao za kujamiiana kwa mara ya kwanza inadhihirisha kwamba kuna tofauti kati ya wanaume na wanawake katika uzoefu na mitazamo juu ya suala la ridhaa au shuruti katika kujamiiana. Wakati karibu wanaume wote wanaojamiiana (asilimia 94) waliripoti kwamba walipojamiiana kwa mara ya kwanza ilikuwa ni kwa “ridhaa” ya pande zote mbili, wanawake wachache ukilinganisha na wanaume (asilimia 77) ndio waliokuwa na maoni sawa na wanaume kuhusu hili. Asilimia ishirini ya wanawake walisema kwamba walipojamiiana kwa mara ya kwanza walikuwa wamelazimishwa au wameshurutishwa, ukilinganisha na asilimia 3 tu ya wanaume waliosema hivyo.

**Katika baadhi ya masuala yanayohusu afya ya uzazi na ujinsia, wanaume na wanawake wanakubaliana kwa kiasi kikubwa**. Kwa mfano, takriban theluthi moja ya wanaume na wanawake waliohojiwa wanadhani kwamba kuzuia mimba ni jukumu la mwanamke, na sio mwanaume. Matokeo haya pia yanaonesha kuwepo kwa mkanganyiko wa mitazamo baina ya wanawake na wanaume kuhusu matumizi ya njia za uzazi wa mpango, na idadi isiyopaswa kupuuzwa ya wanaume na wanawake waliohojiwa walikuwa na mitazamo hasi na imani potofu juu ya njia za kuzuia mimba. Zaidi ya hayo, waliohojiwa — wanaume na wanawake, watu wazima na vijana – wanapinga vikali na

walisema kwamba jamii zao zinapinga vikali suala la wasichana kujamiiana kabla ya ndoa na suala la wanaume kuwa na wenzi wengi, ingawa mitazamo hiyo iliyoripotiwa ni tofauti na hali halisi ya mambo katika jamii zao.

**Wanawake nchini Tanzania wameendelea kubeba mzigo mzito wa shughuli za nyumbani, ingawa wanaume na wanawake hawakubaliani kuhusu ukubwa wa suala hili**. Taarifa za kiasi cha muda ambao watu wanatumia kufanya jambo fulana unaonyesha kwamba kati ya watu wote waliohojiwa – ikiwa ni pamoja na wenzi wanaoishi pamoja bila ndoa na vijana balehe wanaoishi na wazazi wao – wanawake hutumia wastani wa karibu masaa 30 kwa kila wiki katika kufanya kazi za upishi, usafi, kuosha nguo, kuchota maji na kwenda sokoni wakati wanaume hutumia zaidi tu ya masaa 12 kwa kila wiki kufanya kazi hizi. Wakijibu swali lililouliza wana mtazamo gani kuhusu mgawanyo wa kazi katika kaya, asilimia 96 ya wanawake walisema wanafanya kazi nyingi zaidi za nyumbani kuliko wenzi wao, wakati asilimia 68 tu ya wanaume ndio waliokubaliana na hili.

**Ushiriki wa wanaume katika majukumu ya nyumbani una faida kati ya kizazi na kizazi**: Kama inavyojitokeza kila mara katika tafiti duniani kote, wanaume nchini Tanzania ambao baba zao waliwahi kushiriki katika majukumu ya nyumbani wao pia wana uwezekano mkubwa zaidi wa kushiriki katika majukumu haya. Asilimia arobaini na tano ya wanaume ambao baba zao walikuwa wakishiriki katika kazi za nyumbani katika familia walizokulia walisema kwamba wao wenyewe kwa sasa wanafanya majukumu haya, ukilinganisha na asilimia 29 ya wanaume ambao baba zao hawakuwahi kushiriki katika majukumu ya nyumbani.

**Matokeo pia yanathibitisha kwamba — kama ilivyo katika maeneo mengine ambapo tafiti za IMAGES zilifanyika — wanawake waliohojiwa wanafanya sehemu kubwa ya malezi, wanaume wanashiriki kwa kiasi fulani, na wanawake na wanaume wanapingana kuhusu kiwango cha ushiriki wa wanaume**. Wakati asilimia 61 ya wanaume na asilimia 43 ya wanawake waliripoti kwamba wanaume wana mchango sawa au mchango mkubwa zaidi katika malezi na uangalizi wa kila siku wa watoto, idadi kubwa ya wanaume na wanawake walisema kwamba kwa kawaida wanawake ndio wanaofanya majukumu ya kawaida ya malezi ya watoto kama kubadilisha nepi, kulisha na kuogesha watoto. Wanaume, na kwa kiasi kidogo wanawake, waliripoti ushiriki mkubwa wa wanaume katika kuwasimamia watoto kufanya kazi za shuleni, kuzungumza na mtoto kuhusu masuala yanayohusu maisha yake, na kurekebisha tabia za watoto kwa kuwaadhibu au kuzungumza nao. Kwa mfano, asilimia 29 ya wanaume waliripoti kwamba siku zote au kwa kawaida husaidia watoto kufanya kazi za shuleni, wakati asilimia 8 tu ya wanawake ndio walioripoti kwamba wenzi wao hufanya kazi hiyo siku zote. Kwa ujumla, wanaume wana uwezekano mkubwa zaidi kuliko wanawake kuripoti kwamba majukumu ya malezi yanagawanywa sawa kwa sawa baina yao na wenzi wao au hufanywa kwa ushirikiano.

**Nchini Tanzania, kiwango cha wanaume kuwathibiti wanawake katika mahusiano ya kimapenzi ni kikubwa, kama ilivyoripotiwa na wanaume na wanawake**. Wanaume watatu kati ya wanne walioripotiwa kuwa angalau na tabia mojawapo ya udhibiti kwa mpenzi wa sasa au wa hivi karibuni, kwa mfano mwanaume kuwa na nguvu zaidi ya kufanya maamuzi muhimu yanayowahusu wote wawili,

kutaka kujua mahali alipo mwenzi wake kila wakati, au kutarajia mwenzi wake akubali kujamiiana pindi yeye anapohitaji. Wanawake wanne kati ya watano waliripoti kwamba mwenzi alikuwa na angalau mojawapo ya tabia hizi. Wanaume wana uwezekano mdogo kuliko wanawake kuripoti migogoro katika mahusiano. Walipoulizwa ni mara ngapi wanakwaruzana na wenzi wao wa sasa au wa hivi karibuni, wanaume wengi mara mbili zaidi ya wanawake waliripoti kwamba hawakwaruzani na wenzi wao, na asilimia 3 tu ya wanaume (ikilinganishwa na asilimia 19 ya wanawake) waliripoti kwamba hukwaruzana na wenzi wao mara kwa mara. Wanawake wengi pia waliripoti kuwaogopa wapenzi wao — karibu mmoja kati ya wanne (asilimia 23) walisema kwamba wanawahofia wenzi wao mara kwa mara au muda wote.

**Matokeo ya IMAGES Tanzania yanaonesha kiwango kikubwa cha ukatili baina ya wenzi katika kipindi chote cha mahusiano, huku kukiwa na tofauti kubwa kati ya wanaume walioripoti kufanya ukatili na wanawake walioripoti kufanyiwa ukatili**. Wanawake wawili kati ya watano waliripoti kuwahi kufanyiwa ukatili wa kimwili au wa kiuchumi, mmoja kati ya watatu aliripoti kufanyiwa ukatili wa kingono, na zaidi ya asilimia 60 waliripoti kuwahi kufanyiwa ukatili wa kihisia. Kinyume chake, idadi ya wanaume walioripoti kufanya ukatili wa kimwili na wa kihisia ni nusu ya idadi ya wanawake walioripoti kufanyiwa ukatili huo; kuhusu ukatili wa kingono, wanaume walioripoti kufanya ukatili huo ni wachache karibu mara kumi chini ya wanawake walioripoti kufanyiwa ukatili huo. Kwa kuwa viwango vya ukatili vilivyoripotiwa na wanawake vinafanana na tafiti nyingine zilizofanyika nchini Tanzania, inawezekana kwamba wanaume wengi hawakiri kufanya ukatili. Hii inaweza kuhusishwa na mambo kadhaa, ikiwemo utayari wa jamii kujibu maswali katika dodoso na uelewa kuhusu ongezeko la juhudi za kupambana na ukatili; viwango hivi vinapaswa kutafsiriwa kwa tahadhari na kwa kuangalia ripoti za wanawake ambazo zinatoa picha ya ukubwa wa tatizo.

**Katika jumla ya maeneo ambayo utafiti wa IMAGES ulitazama, watu waliohojiwa kwa kiasi kikubwa waliripoti mitazamo chanya na utayari wa mabadiliko kuliko matarajio ya kitabia na kimitazamo katika jamii zao**. Inawezekana kwamba, kwa mujibu wa utafiti huu, watu waliohojiwa walitaka kuonekana wanaamini katika usawa wa kijinsia na walitaka kuonesha kile wanachohisi kwamba "ni sahihi zaidi katika jamii". Hata hivyo, inawezekana pia kwamba kuna tofauti kati ya mitazamo binafsi na mitazamo ya kijamii, jambo ambalo linaendana na matokeo ya utafiti wa kupima ubora (*qualitative*) ambayo yanaonesha uwepo wa wingi wa maoni na uzoefu tofauti. Tofauti hizi kati ya mitazamo binafsi na mitazamo ya kijamii ni fursa muhimu ya mabadiliko.

## MWELEKEO

Matokeo ya IMAGES Tanzania yanaainisha maeneo muhimu ya kufanyia kazi katika agenda ya kuleta usawa wa kijinsia nchini. Mapendekezo ya hatua za muda mfupi na za muda wa kati kutokana na matokeo haya ni pamoja na:

- **Kuunganisha juhudi za kuleta usawa wa kijinsia na uhakika wa kipato**: Utafiti wa IMAGES Tanzania unaonyesha viwango vikubwa vya shida za kiuchumi ambazo zimeripotiwa na wanaume pamoja na wanawake. Programu za usawa wa kijinsia na vita dhidi ya ukatili

nchini Tanzania, kama ilivyo katika sehemu nyingine nyingi, zitakuwa na mafanikio makubwa kama zitashughulikia pia tatizo la ukosefu wa uhakika wa chakula na changamoto za kiuchumi, kwa mfano, kwa kutoa pesa, chakula, vitu au kuwawezesha watu kuanzisha shughuli za uzalishaji mali.

- **Kukuza tabia na mitazamo chanya iliyopo kuhusu usawa wa kijinsia pamoja na kurithisha vizazi hadi vizazi**: IMAGES Tanzania imegundua kwamba watu ambao mama zao wana elimu, baba zao wana elimu au baba zao wanakuwa na mamlaka sawa na wenzi wao katika kufanya maamuzi – pamoja na wanaume wanaopata taarifa katika vyombo vya habari — wana mitazamo chanya zaidi kuhusu usawa wa kijinsia. Tanzania imepiga hatua kiasi fulani katika suala la usawa wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na mabadiliko miongoni mwa wanaume, na kampeni, mipango na sera zinapaswa kusisisitiza na kuongeza msukumo wa mafanikio haya, kwa kujikita katika malezi yanayofundisha heshima na usawa. Mbinu chanya zinazohamasisha na kuhimiza imani za wanaume juu ya usawa wa kijinsia zina nafasi kubwa ya kuzaa matunda.

- **Kutumia mabadiliko ya desturi yaliyokwishapokelewa na jamii katika kubuni kampeni na mikakati ya kupambana na ukatili**: Uchache wa wanaume wanaokiri kufanya ukatili dhidi ya wenzi wao ukilinganisha na idadi ya wanawake walioripoti kufanyiwa ukatili unaonyesha kwamba wanaume wanafahamu kwamba ukatili ni jambo lisilokubalika katika jamii. Ingawa kuna mtazamo kwamba desturi zinabadilika, mabadiliko haya yanaweza yasitoshe kukomesha vitendo vya ukatili wa wanaume dhidi ya wanawake. Hata hivyo, mbinu za kubadili desturi katika jamii, zinaweza kujenga msingi imara kwa wale wasiochukua hatua au mikakati inayohusiana na kuelimisha wanaume kufanya jambo ambalo wanalijua au wanaona ni "sahihi". Kampeni zijazo zinazolenga wanaume zinaweza kusisitiza kwamba: "Unakubali kwamba ukatili ni jambo baya. Sasa, tuutokomeze."

- **Kuhusisha akinababa katika kuhakikisha vijana wanapata huduma na haki na afya ya uzazi na ujinsia**: Kwa ujumla, wanaume wanaunga mkono vijana kupata na kutumia njia za kuzuia mimba, hivyo kuna haja ya kuhusisha akinababa, sambamba na akinamama, katika kuhamasisha haki na afya ya uzazi na ujinsia kwa vijana, ikiwemo kuwasaidia vijana kufanya maamuzi kuhusu ujinsia na matumizi ya njia za kuzuia mimba.

- **Kuendeleza mabadiliko chanya ya kimitazamo ili kuleta mabadiliko ya desturi katika jamii**: Wanawake na wanaume mara nyingi wana mitazamo inayolingana na wanaunga mkono suala la usawa wa kijinsia kuliko wanavyomchukulia mtu mmojammoja katika jamii zao. Hii inatoa fursa kubwa ya kuendeleza utayari wa wanaume na wanawake kupinga desturi mbaya, pamoja na kuandaa kampeni za kijamii na za kitaifa zinazosisitiza kwamba watu wengi binafsi tayari wanaunga mkono usawa wa kijinsia.

- **Kukomesha ukatili katika mahusiano ya kimapenzi ni pamoja na kuwa na mikakati madhubuti inayowalenga wazazi na wenzi**: IMAGES Tanzania imegundua kwamba

kushuhudia ukatili, ugomvi, au migogoro mikubwa ya kimahusiano na ya kiuchumi baina ya wenzi kipindi cha utotoni inahusiano mkubwa na wanaume kuwa wakatili dhidi ya wanawake. Hii inaonesha umuhimu wa mikakati inayolenga jamii na wenzi, ambayo itaboresha mawasiliano na mamlaka sawa baina na wenzi, pamoja na mikakati inayohusisha shughuli za uzalishaji mali au uwezeshaji wa kiuchumi. Zaidi ya hayo, viwango vikubwa vya kukubalika, kukiri kufanya ukatili, na ukatili dhidi ya watoto — pamoja na idadi kubwa ya wanawake walioripoti kuwahi kufanyiwa ukatili na wenzi wao, na idadi ndogo ya wanaume wanaoripotiwa kushiriki katika malezi ya watoto — vinaonesha umuhimu wa mikakati inayolenga kuzuia ukatili ambayo inahusisha mafunzo kwa wazazi yenye lengo la kuleta usawa wa kijinsia.

- **Kumbuka kwamba akinababa wa Kitanzania wanahudumia na wanataka kuhudumia**: Kuhudumia watoto ni kazi ya nyumbani ambayo wanaume wengi wameripoti kushiriki na ni kazi ambayo ina kiwango kidogo zaidi cha unyanyapaa, jambo ambalo linathibitisha kwamba kuhamasisha ushiriki sawa wa wanaume katika malezi ya watoto na wanakaya wengine inawezakuwa mojawapo ya mikakati madhubuti ya kuhamasisha usawa wa kijinsia na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza ukatili dhidi ya watoto na wanawake nchini Tanzania.

## REJEA



ICF. (2015). *Data from Tanzania DHS 1991-92, 2004-05, and 2015-16.* In STATcompiler. Retrieved June 20, 2018, from http://www.statcompiler.com

Tanzania Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly, and Children (MoHCDGEC); Ministry of Health Zanzibar; Tanzania National Bureau of Statistics; Tanzania Office of the Chief Government Statistician; & ICF. (2016). *Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015-16.*

United Nations Children's Fund (UNICEF). (2011). *Adolescence in Tanzania.* Dar es Salaam: United Nations Children's Fund.

United Nations Children's Fund (UNICEF), United States Centers for Disease Control and Prevention (CDC); & Muhimbili University of Health and Allied Sciences (MUHAS). (2011). *Violence against children in Tanzania: Findings from a national survey, 2009. Summary report on the prevalence of sexual, physical and emotional violence, context of sexual violence, and health and behavioural consequences of violence experienced in childhood.* Dar es Salaam, Tanzania: United Nations Children's Fund Tanzania Division of Violence Prevention, United States Centers for Disease Control and Prevention National Center for Injury Prevention and Control, & Muhimbili University of Health and Allied Sciences.

United Nations Development Programme (UNDP). (n.d.). *Human Development Reports: Table 5: Gender Inequality Index.* Retrieved June 21, 2018, from http://hdr.undp.org/en/composite/GII



PROMUNDO

UMATI
For Choice and Opportunities
Member of IPPF